JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**
ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 10 - 2020/2021**

**DHIDI YA**

## ABOOD FM RADIO

# UAMUZI

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI KUHUSU TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI WA REDIO NA TELEVISHENI), 2018.**

## 1.0 MAELEZO KUHUSU UKIUKAJI WA KANUNI

1.1 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ilitoa leseni ya kurusha Matangazo (Matangazo ya Redio) kwa Kituo cha **Abood FM Radio** kwa ajili ya kutoa huduma ya utangazaji wa maudhui kwa njia ya redio.

1.2 Tarehe 29 Julai, 2020 kati ya Saa 12.00 na Saa 12.30 asubuhi, Kituo cha **Abood FM Radio** kinatuhumiwa kukiuka Kanuni na Maadili ya Utangazaji kupitia kipindi cha ***Amka na BBC*** kwa kurusha maudhui bila kuzingatia mizania ya habari pale walipokuwa wakimhoji Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Bw. Tundu Lissu juu ya viongozi wa chama hicho kutoshiriki katika kutoa heshima za mwisho kwa aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Benjamin William Mkapa.

1.3 Mtangazaji wa kipindi hicho wakati akimhoji Bw. Tundu Lissu aliruhusu kurushwa kwa habari iliyoegemea upande mmoja pale Bw. Tundu Lissu alipotoa tuhuma na kulalamika kuwa Serikali ilimnyima nafasi ya kutoa heshima za mwisho kwa Hayati Benjamin William Mkapa, bila kumtafuta Msemaji wa Serikali ili aweze kutolea ufafanuzi tuhuma hizo, jambo ambalo ni kinyume na Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

1.4 Wakati wa kipindi cha ***Amka na BBC***, Bw. Tindu Lissu alisikika akizungumza maneno yafuatayo:

***"...Inasikitisha sana, tumefika kwa wakati tulioambiwa kwa mujibu wa ratiba. Kutuambia kwamba hatuwezi kuingia uwanjani kwa sababu tumechelewa tuliona ilikua ni namna tu ya kusema kwamba hawataki tushiriki kumuaga huyu aliyekuwa Rais wetu...Haiwezekani tena kama hutakiwi na waandaaji wa msiba ukilazimisha kwenda watakwambia wewe ndo mchawi. Sisi hatutaki kuonekana ni wachawi wa mzee Mkapa tumesema waendelee tu Mungu awabariki.".***

## 2.0 KANUNI ZILIZOKIUKWA

Kitendo cha **Abood FM Radio** kurusha kipindi kilichoituhumu Serikali bila ya kuthibitisha ukweli wa madai yaliyotolewa katika taarifa hiyo kutoka kwenye vyanzo husika na kutozingatia mizania, **Abood FM Radio** wanatuhumiwa kukiuka Kanuni Na.15(2) (b) na (c) na Na. 16 za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018; ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

*15. (2) The licensee shall-*

*(b) report accurately, impartially, fairly and in a non- partisan manner;*

*(c) report news in an objective and balanced manner, without intentional or negligent departure from the facts, whether by distortion, exaggeration, misrepresentation or material omission.*

*16. A content service licensee shall ensure that, during the presentation of current affairs programme, factual programmes and documentaries; where issues of public importance are discussed, reasonable effort is made and reasonable opportunity is given to present a fair, accurate, balanced and impartial view.*

## 3.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI.

Tarehe 05 Agosti, 2020, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Abood FM Radio** wito wa kuwasilisha utetezi wao wa maandishi pamoja na kufika mbele ya Kamati ya Maudhui kujieleza dhidi ya tuhuma zinazowakabili.

Tarehe 10 Agosti, 2020, Uongozi wa **Abood FM Radio** uliwasilisha utetezi wa maandishi uliosainiwa na **Abedi Saidi Dogoli**, Meneja wa **Abood FM Radio.** Pia, tarehe hiyo hiyo, Uongozi huo ukiwakilishwa na **Abedi Saidi Dogoli** na **Rayson Elijah Luka**, Wakili wa **Abood FM Radio** ulifika mbele ya Kamati kutoa utetezi.

## 4.0 KUSOMEWA SHITAKA NA KUSIKILIZA MAUDHUI YA ABOOD FM RADIO

Kamati ya Maudhui iliusomea Uongozi wa **Abood FM Radio** shitaka lao. Pia, Kamati ya Maudhui na Uongozi wa **Abood FM Radio** walisikiliza maudhui yaliyotangazwa na **Abood FM Radio** katika tarehe tajwa hapo

juu na kisha kuualika Uongozi huo kujitetea ili kujiridhisha iwapo maudhui hayo yalikiuka Kanuni.

## 5.0 UTETEZI WA ABOOD FM RADIO

Katika maelezo yao ya maandishi**, Abood FM Radio** walipinga mashitaka husika ya kwamba taarifa iliyotolewa inakiuka Sheria za nchi na kudai kuwa **Abood FM Radio** kupitia matangazo ya **BBC** imetoa taarifa inayoyalalamikiwa kwa kutimiza matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 18, wanayodai kuwa inatoa uhuru wa kila mtu kupokea na kutoa habari na dhana zo zote kupitia chombo cho chote bila ya kujali mipaka ya nchi.

Walisema kuwa **Abood FM Radio** ina mkataba wa kurusha vipindi vya **BBC** na moja ya matakwa ya mkataba huo ni kwamba **Abood FM Radio** hawapaswi kubadili cho chote katika maudhui wanayopokea kutoka **BBC**, kwani **BBC** wana jukumu la kuhakikisha kuwa habari iliyotangazwa imezingatia Maadili yote ya Uandishi wa Habari ikiwemo mizania. Walinukuu kipengele husika cha mkataba wao kama ifuatavyo:

***"...We licence the content from the BBC. In the Licence Agreement which we've signed, the BBC warrants that the content complies with editorial guidelines, which means that each programme must be amongst other things balanced. We Abood Media agree under the terms of the same Agreement, not to edit or amend any of the content, we must broadcast it in full as we receive it from the BBC in London".***

Waliendelea kudai kuwa madai ya Kamati dhidi yao si ya kweli kwa sababu **Abood FM Radio** kupitia matangazo ya **BBC** imetoa habari kwa usahihi kwani habari waliyoitoa ni ya mahojiano na mhusika mwenyewe. Pia, walidai kwamba BBC waliwaeleza kuwa habari inayolalamikiwa imefuata Kanuni zote za Uandishi na Utangazaji wa Habari kwa kuwa juhudi za kuhakikisha inapata maelezo ya Msemaji wa Serikali zilifanyika bila ya mafanikio. Pia, walieleza kuwa habari hiyo ilikuwa ni muendelezo wa habari ambayo alihojiwa Msemaji wa CHADEMA na kwamba katika habari hiyo ya awali, mtangazaji alieleza kuwa jitihada za kumtafuta Msemaji wa Serikali zinaendelea.

Walimalizia kwa kusema kuwa wanaiomba Kamati ione kwamba taarifa iliyotolewa na Kituo chao kupitia matangazo ya **BBC** ilizingatia Kanuni zote za Utangazaji. Kwamba taarifa hiyo haikuwa na lengo la kuegemea upande wo wote na juhudi za kuutafuta upande wa pili zilifanyika bila mafanikio. Hata hivyo, **BBC** wanaendelea kuwatafuta wasemaji wa upande wa pili. Pia, waliiomba Kamati itupilie mbali tuhuma dhidi yao na kwamba watawaambia washirika wao kuwa katika habari zote wanazowaletea wazingatie mizania ili kuepusha migogoro.

Pia, **Abood FM Radio** ilitoa utetezi wao wa mdomo kama ifuatavyo:

5.1 **Abedi Saidi Dogoli,** alipoulizwa na Kamati, alijibu kuwa wameliona kosa walilolifanya na wanalifanyia kazi. Pia, alisema kuwa wapo katika taratibu za kuongea na vyombo vyote vya habari vya nje ya nchi walivyo na mikataka navyo ya kurusha maudhui yao ili wawe wanawaletea vipindi/maudhui yanayozingatia Sheria, Kanuni na maadili ya tasnia ya habari.

5.2 **Rayson Elijah Luka** alisema kuwa Utetezi wao wa maandishi na mdomo hautofautiani bali wanamaanisha kuwa jitihada za kuweka mizania kwenye habari yao zilifanyika, lakini iwapo Kamati itaona kuwa jitihada zao hazikutosha, basi wanaomba wapatiwe adhabu ndogo ya Onyo kwa sababu Kamati ni kama mlezi wao. Pia, alisema kuwa wanakubali kulikuwa na udhaifu wa kushindwa kutoa taarifa ya kila kilichokuwa kinaendelea katika jitihada zao za kujaribu kutafuta mizania ya taarifa yao.

## 6.0 TATHMINI YA KAMATI

6.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Abood FM Radio** imetenda kwa uzembe kosa la kutangaza maudhui bila ya kuzingatia mizania ya habari kwa kushindwa kufanya juhudi za kutoa fursa kwa Serikali kutolea ufafanuzi tuhuma dhidi yake.

6.2 Kamati ya Maudhui imeona kuwa utetezi wa **Abood FM Radio** kuwa taarifa yao ilizingatia matakwa ya Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya kwamba kila mtu ana uhuru wa kupokea na kutoa habari na dhana zo zote kupitia chombo cho chote bila ya kujali mipaka ya nchi, hauna msingi wo wote kwa sababu kwa mujibu wa Ibara hiyo hiyo ya 18, Katiba haijatoa uhuru usiokuwa na mipaka (absolute freedom) bali Ibara hiyo inamtaka mtu kutumia uhuru huo bila kuathiri matakwa ya Sheria nyingine za nchi. Hivyo, **Abood FM Radio** walipaswa kutumia uhuru huo kwa kuhakikisha hawavunji Sheria na Kanuni zinazosimamia chombo chao;

6.3 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba utetezi wa **Abood FM Radio** kuwa mkataba wao na **BBC** unawataka kutobadili cho chote katika maudhui wanayopokea kutoka **BBC,** hauna mashiko yo yote kwa sababu **Abood FM Radio** ndio wanamiliki leseni ya Utangazaji wa Habari hapa nchini, hivyo **Abood FM Radio** wana wajibu wa kuhakikisha kuwa maudhui yote wanayotangaza, yaliyozalishwa hapa nchini au wanayopokea kutoka vyombo vya habari vya nje ya nchi, yanazingatia Sheria, Kanuni, Weledi na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari, masharti ya leseni yao pamoja na Maadili na Utamaduni wa Kitanzania;

6.4 Kamati ya Maudhui imeona kuwa utetezi wa **Abood FM Radio** kuwa **BBC** walifanya jitihada za kumtafuta Msemaji wa Serikali lakini hazikufanikiwa na kwamba jitihada zilikuwa zinaendelea, hauna mashiko kwa sababu wao, **Abood FM Radio** waliotangaza habari ile kupitia chombo chao ndiyo walitakiwa kufanya jitihada za kupata maoni ya Serikali.

6.5 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba hoja ya **Abood FM Radio** kwamba bado **BBC** wanaendelea kumtafuta Msemaji wa Serikali ili kuweka mizania katika habari yao ni utetezi dhaifu kwa sababu zimepita wiki mbili tangu warushe tuhuma hizo.

6.6 Kamati ya Maudhui imeona kuwa hoja ya **Abood FM Radio** kuwa taarifa inayotuhumiwa ilikuwa ni muendelezo wa habari ambayo alihojiwa Msemaji wa CHADEMA, haina msingi wo wote kwa sababu katika taarifa zote mbili, kila taarifa ilikuwa inajitegemea na hivyo walitakiwa kuzingatia matakwa ya kisheria ya kuweka mizania katika taarifa yao.

6.7 Kamati ya Maudhui imebaini kuwa **Abood FM Radio** wana Usimamizi dhaifu wa vipindi vyao hasa wanavyopokea na kuvirusha kutoka vyombo vya habari vya nje ya nchi, jambo lililofanya watangaze habari isiyokidhi matakwa ya kisheria.

6.8 Kamati imeona kuwa mkataba waliojifunga **Abood FM Radio** na **BBC** ambao unawataka **Abood FM Radio** kutangaza maudhui wanayopokea kutoka **BBC** kama yalivyo, una mapungufu makubwa kwani unaweza kusababisha kutumbukia katika maudhui yanayokinzana na sheria, Kanuni, maadili na utamaduni wa Mtanzania.

6.9 Hivyo, Kamati ya Maudhui imeridhika kuwa **Abood FM Radio** imetenda kosa la kurusha kipindi kilichoituhumu Serikali bila ya kuthibitisha ukweli wa madai yaliyotolewa katika taarifa hiyo kutoka kwenye vyanzo husika na kutozingatia mizania ya Uandishi na Utangazaji wa Habari, kinyume na Kanuni Na. 15(2) (b) na (c) na Na. 16 za Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni) 2018;

## 7.0 USHAURI WA KAMATI KWA ABOOD FM RADIO

Kutokana na makosa yaliyobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Abood FM Radio** kuimarisha Usimamizi wa maudhui yao ili kuepuka utangazaji wa maudhui yanayovunja Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari;

Pia, **Abood FM Radio** wanashauriwa kupitia upya mikataba yao na vyombo ya utangazaji wa habari vya nje ya nchi ili kuhakikisha masharti ya mikataba yao yanazingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya Uandishi na Utangazaji wa Habari pamoja na masharti ya leseni yao.

## 8.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kuutafakari kwa kina utetezi uliotolewa na Uongozi wa **Abood FM Radio**, Kamati ya Maudhui imeridhika pasi na shaka kuwa **Abood FM Radio** wamekiuka Kanuni tajwa za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018.

Hivyo basi, Kamati ya Maudhui inatoa adhabu zifuatazo kwa **ABOOD FM RADIO:**

1. Wanapewa Onyo Kali;

2. Wanawekwa chini ya uangalizi kwa muda wa miezi sita (6) pamoja na kutahadharishwa kuwa hatua kali zaidi za kisheria zitachukuliwa dhidi yao iwapo hawatajirekebisha na kurudia makosa kama hayo ndani ya muda tajwa.

Uamuzi huu umetolewa Dar es Salaam, leo tarehe **14 Agosti, 2020**.

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani wa Haki Kibiashara (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku 21 (ishirini na moja) kuanzia siku ya kutolewa kwa uamuzi huu.

**Uamuzi huu umesainiwa na:**

**Joseph Method Mapunda**

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA,
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

..................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui**

**PAMOJA NA WAJUMBE WAFUATAO WA KAMATI YA MAUDHUI:**

1. **Abdul Ramadhani Ngarawa**..................................
2. **Derek Kaitira Murusuri**..................................
3. **Jacob Gregory Tesha**..................................